HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 17/01/2022 KATIKA OFISI YA AFISA MIPANGO

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

1. GILBERT A. NGAILO – AFISA ARDHI NA MALIASILI (W) – MWENYEKITI
2. KEVIN N. KUSENGE – AFISA MANUNUZI (W) – KATIBU
3. THOMAS C. KIOWI – AFISA MAENDELEO YA JAMII (W) – MJUMBE
4. STANLEY A. MLAY - MGANGA MKUU (W) - MJUMBE
5. ADILI V. KAYOMBO - AFISA MIPANGO - MJUMBE
6. CASTOR G. KIBASSA – AFISA USAFI NA MAZINGIRA (W)

**MSHAURI**

1. MATHAN CHALAMILA – MWANASHERIA (W) – MSHAURI

**SEKRETARIETI**

1. HILMALA KALASO - MWANDISHI WA VIKAO

**AGENDA NAMBA 01/01/2021 – 2022 – KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kuwaeleza kuwa kikao hiki ni kikao cha kawaida kwa ajili ya kujadili na kisha kutolea maamuzi masuala mbalimbali yanayohusu manunuzi ya vifaa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na miradi mingine mbalimbali inayoendelea katika Wilaya yetu ya Ludewa.
Mwenyekiti baada ya kusema hayo alifungua kikao saa 06:30 mchana

**AGENDA NAMBA 02/01/2021 – 2022 – KUPOKEA AGENDA**

Agenda kumi (10) ziliwasilishwa ambapo agenda zote 10 zilipokelewa kwa ajili ya kujadiliwa , agenda hizo ilikuwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao
2. Kupokea agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 01/09/2021
4. Mapendekezo ya kuiteua kampuni ya Dangote Cement kuiuzia Halmashauri mifuko 4,200 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Boma
5. Mapendekezo ya kuiteua kampuni ya Madunda Construction kwa ajili ya kuiuzia Halmashauri kokoto mita za ujazo 312 zenye thamani ya Tshs 59,592,000/- kwa matumizi ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya boma
6. Mapendekezo ya kuiteua kampuni ya Kalumanyili Enterprises kwa ajili ya kuiuzia Halmashauri nondo , marine board , master seal na misumari ya zege kwa matumizi ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya boma



Scanned with CamScanner

7. Mapendekezo ya kuiteua kampuni ya Kalumanyil Enterprises kwa ajili ya ujenzi wa kichomea taka katika kituo cha Afya Makonde.

8. Mapendekezo ya kutumia utaratibu wa 'FORCE ACCOUNT' katika miradi ya ujenzi wa madarasa 47 , ujenzi nyumba ya mtumishi three in one na jengo la wagonjwa mahututi

9. Mapendekezo ya kumteua mzabuni Flowin Mkinga kuiuzia mbao Halmashauri za 2x2x12 vipande 500 na 2x3x12 vipande 500 kwa Tshs 3,100,000/=
10. Kufunga kikao

**AGENDA NAMBA 03/01/2021 - 2022 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 01/09/2021**

Muhtasari wa tarehe 01/09/2021 ulisomwa na wajumbe waliupitia ukurasa kwa ukurasa ili kuufanyia masahihisho katika ukurasa wa kwanza neno ''katbu'' lilisahihishwa na kuwa katibu na baada ya masahihisho hayo muhtasari ulithibitishwa kuwa ni sahihi na kusainiwa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao

**AGENDA NAMBA 04/01/2021 – 2022 – MAPENDEKEZO YA KUITEUA KAMPUNI YA DANGOTE CEMENT KUIUZIA HALMASHAURI MIFUKO 4,200 YA SARUJI KWA AJILI YA UJENZI WA OFISI ZA BOMA**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa kwa sasa kuna hitaji la kununua saruji mifuko 4,200 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi za Boma. Katika kufanikisha manunuzi haya Katibu alieleza kuwa tayari amepata nukuu ya bei toka kiwanda cha Dangote Cement ambapo bei ya mfuko mmoja pamoja na VAT ni Tshs 14,690/= ambapo gharama ya mifuko yote 4,200 inakuwa 61,698,000/=. Hivyo basi kitengo cha Manunuzi kinapendekeza saruji mifuko 4,200 inunuliwe toka kiwandani kwa mzabuni Dangote Cement kwa gharama ya Tshs 61,698,000/=.
Baada ya kusema hayo Katibu aliwasilisha.

**MAAMUZI YA BODI YA ZABUNI**
Wajumbe wa Bodi ya Zabuni waliyapitia mapendekezo haya na kusema kuwa endapo saruji mifuko 4,200 itanunuliwa toka kiwandani Halmashauri itaokoa kiasi kikubwa sana cha fedha kwani bei ya mfuko mmoja kwa wazabuni wengine ni Tshs 18,000 lakini kiwandani ni Tshs 14,690/=, pia wajumbe waliagiza kuwa baada ya malipo ufanyike ufuatiliaji wa karibu ili saruji iweze kuletwa mapema .
Wajumbe waliridhia na kuamua kuwa saruji mifuko 4,200 kwa bei ya Tshs 14,690/- kwa mfuko itakayogharimu kiasi cha Tshs 61,698,000/- inunuliwe toka kiwanda cha Dangote Cement.



Scanned with CamScanner

**MAAMUZI YA BODI YA ZABUNI**
Wajumbe wa Bodi ya Zabuni waliridhia na kukubali kuwa vifaa vya ujenzi vinunuliwe toka kwa mzabuni Kalumanyili Enterprises S.L.P 894 Iringa kwa gharama ya Tshs 174,458,500/= na ufuatiliaji ufanyike ili vifaa hivyo viletwe kwa wakati.

**AGENDA NAMBA 07/01/2021 - 2022 - MAPENDEKEZO YA KUITEUA KAMPUNI YA KALUMANYILI ENTERPRISES KWA AJILI YA UJENZI WA KICHOMEA TAKA KATIKA KITUO CHA AFYA MAKONDE**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa hadi sasa kituo cha Afya cha Makonde hakina kichomea taka kizuri kilicho katika viwango hivyo basi Halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kichomea taka katika kituo cha Afya Makonde ili kukamilisha idadi ya majengo matano na mradi uanze kutumika.
Katika kufanikisha jambo hili Kitengo cha Manunuzi kimetoa hati maulizo tatu na tayari wazabuni wamezirejesha kama ifuatavyo :-

1. Madunda Construction S.L.P 98 Ludewa alitaja kiasi cha Tshs 19,462,000/=
2. Kalumanyili Enterprises S.L.P 894 Iringa alitaja kiasi cha Tshs 13,721,600/=
3. Angeles Engineering S.L.P 70 Ludewa alitaja kiasi cha Tshs18,329,900/=

Baada ya kusema hayo Katibu aliwasilisha.

**MAAMUZI YA BODI YA ZABUNI**
Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walizipitia hati maulizo tatu zilizowasilishwa na kushauri kuwa matengenezo yafanyike kwa haraka mzabuni asimamiwe ili kutengeneza kichomea taka kilicho na ubora .
Wajumbe waliridhia na kukubali kuwa kichomea taka kijengwe na mzabuni Kalumanyili Enterprises S.L.P 894 Iringa kwa gharama ya Tshs 13,721,600/=

**AGENDA NAMBA 08/01/2021 - 2022 - MAPENDEKEZO YA KUTUMIA UTARATIBU WA 'FORCE ACCOUNT' KATIKA MIRADI YA UJENZI WA MADARASA 47, UJENZI NYUMBA YA MTUMISHI THREE IN ONE NA JENGO LA WAGONJWA MAHUTUTI**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs 1,280,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa majengo katika sekta ya Elimu na Afya , Katibu aliendelea kusema kuwa ujenzi wa madarasa 47 umetengewa kiasi cha Tshs 940,000,000.00 , ujenzi wa nyumba ya mtumishi three in one umetengewa kiasi cha Tshs 90,000,000.00 na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi umetengewa kiasi cha Tshs 250,000,000.00.
Hivyo mapendekezo yanawasilishwa katika kikao cha Bodi ya Zabuni ili kuridhia utaratibu wa kutekeleza miradi hii kwa njia ya Force Acccount.

**MAAMUZI YA BODI YA ZABUNI**
Wajumbe waliipitia taarifa hii na kuridhia na kuamua kuwa miradi ya ujenzi ya UVIKO 19 ya madarasa 47 , mradi wa ujenzi wa nyumba ya mtumishi three in one na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi itekelezwe kwa njia ya FORCE ACCOUNT.



Scanned with CamScanner

**AGENDA NAMBA 09/01/2022 - 2022 - MAPENDEKEZO YA KUMTEUA MZABUNI FLOWIN MKINGA KUIUZIA MBAO HALMASHAURI ZA 2X2X12 VIPANDE 500 NA 2X3X12 VIPANDE 500 KWA TSHS 3,100,000/=**

Katibu aliwasilisha taarifa ya ununuzi wa mbao kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Boma , alisema kuwa hati maulizo tatu zimewasilishwa toka kwa wazabuni kwa ajili ya ununuzi wa mbao kama ifuatavyo :-

1. Flowin Mkinga S.L.P 19 Ludewa alitaja kiasi cha Tshs 3,100,000/=
2. Oscar Chaula S.L.P 19 Ludewa alitaja kiasi cha Tshs 3,200,000/=
3. Bethod Mdenye wa S.L.P 19 Ludewa alitaja kiasi cha Tshs 3,250,000/=

Baada ya kusema hayo katibu aliwasilisha .

**MAAMUZI YA BODI YA ZABUNI**

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni waliamua na kuridhia kuwa mzabuni Flowin I Mkinga S.L.P 19 Ludewa aiuzie Halmashauri mbao 500 za 2X3x12 na mbao 500 za 2X4x12 jumla ya mbao 1,000 kwa gharama ya Tshs 3,100,000/=

**AGENDA NAMBA 10/01/2021 – 2022: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao kikamilifu na kuweza kuchangia mawazo yao katika agenda zilizokuwepo mezani kwa ukamilifu , baada ya kusema hayo alifunga kikao saa 07.55 mchana.

**UMETHIBITISHWA**

Saini............................................
Jina Gilbert Ngailo
**Mwenyekiti**

Saini............................................
Jina Kevin N. Kulenge
**Katibu**

Tarehe 22/4/2022



Scanned with CamScanner